# Ushairi wa Mnyampala kama Hifadhi ya Historia ya Jamii ya Tanzania

*Anna Nicholaus Kyamba, Mosol Kandagor* na *Magdaline N. Wafula*
*Chuo Kikuu cha Moi, Kenya*

**Ikisiri**

**Ushairi wa Kiswahili una historia ndefu kuliko tanzu zote za fasihi andishi ya Kiswahili. Kutokana na historia hiyo, utanzu huu umeweza kutumiwa na waandishi mbalimbali katika kuhifadhi historia ya jamii na taifa kwa ujumla. Wataalamu wengi hasa wa tendi na ushairi mara nyingi hutumia tungo hizo, kueleza visa vya kihistoria. Waandishi walioandika kuhusu tenzi wameweza kuonesha historia nzima ya Tanzania na kutupa picha nzima ya vipindi mbalimbali vilivyopitiwa na Tanzania tangu ukoloni mkongwe na Kiarabu, Kijerumani, uhuru hadi Azimio la Arusha. Hata hivyo, wapo waandishi wengi wa Kiafrika walioandika kazi za ushairi wa Kiswahili, kabla na baada ya uhuru wakionyesha picha halisi iliyokuwepo katika jamii ya Watanzania kipindi hicho na kuonesha historia za watu mashujaa waliopinga udhalimu uliokuwa ukifanywa na wakoloni. Kadhalika, kutokana na uchunguzi wetu wa awali, kupitia ushairi wa Mathias Mnyampala, historia ya taifa la Tanzania imejibainisha zaidi. Mazingira hayo yametuchochea kutafiti zaidi ushairi wa Mnyampala na kuona namna historia ya Tanzania inavyojibainisha kwa uwazi. Hivyo basi, makala haya yanakusudia kuchunguza dhima ya ushairi wa Mnyampala katika kuhifadhi historia ya jamii kwa kuchambua kazi za ushairi za Mnyampala.**

**Maneno Muhimu:** Ushairi, Tanzania, Ukoloni, Uhuru

## Utangulizi

Katika makala haya, tunaangazia namna Mnyampala anasawiri matukio na masuala ambayo yaliishughulisha jamii katika kipindi cha utunzi wa kazi zake za ushairi. Kwa hivyo, ushairi wake unaakisi kwa kiasi fulani uhalisi wa jamii yake ya Wagogo na Tanzania kwa ujumla. Vilevile kwa kiasi fulani matukio ya kiulimwengu yanajitokeza katika kazi zake. Ushairi wa Kiswahili una dhima mbalimbali katika jamii. Mojawapo ya dhima za ushairi wa Kiswahili ni kuelimisha, kuburudisha na kurithisha amali za jamii kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine. Kwa ujumla amali za jamii huweza kupatikana kupitia kwa masimulizi mbalimbali. Ushairi wa Kiswahili umetokana na fasihi simulizi ambapo mashairi na tendi nyingi husimulia visa mbalimbali vya jamii au

taifa na kuchangia kuhifadhi historia ya jamii kwa njia ya maandishi. Mmbaga (1978) anaeleza kuwa tangu karne ya 18, tenzi nyingi zenye kuonesha historia ya jamii zimekuwa zikijidhihirisha. Mmbaga anatoa mfano wa *Utenzi wa Uhuru wa Tanganyika* ulioandikwa na Mwinyihatibu, *Utenzi wa Jamhuri ya Zanzibar* ulioandikwa na Salim A. Kibao, *Utenzi wa Jamuhuri ya Tanzania* ulioandikwa na Ramadhani Mwaruka. Kimsingi, tenzi hizo zilitungwa kuelezea historia ya Tanganyika na Zanzibar. Aidha, waandishi wengi waliandika kazi zao kwa kuegemea kipindi mahususi ambacho walikuwepo, wengi wao waliweza kuangalia historia nzima ya Tanzania na kuiweka kimaandishi kwa muundo wa kishairi. Mnyampala ni miongoni mwa waandishi waliokuwa katika mstari wa mbele kukuza na kuendeleza ushairi wa Kiswahili na kwa njia hiyo akaweza kuhifadhi historia ya jamii ya Tanzania. Katika mashairi ya Mnyampala, aliweza kuangazia historia nzima ya Tanzania na kutoa picha kamili ya vipindi vyote ambavyo jamii ya Tanzania ilipitia tangu harakati za kupigania uhuru, muungano na wakati wa Azimio la Arusha. Vilevile, katika mashairi yake amezungumzia madhila ya ukoloni dhidi ya Watanzania yanamulika hali na jitihada za mashujaa wa Tanzania na Afrika kwa ujumla.

Makala haya yamekitwa kwenye misingi ya nadharia ya Uhistoria Mpya. Hii imetokana na sababu kuwa Uhistoria Mpya ni nadharia ambayo inachunguza umuhimu wa muktadha katika kuhakiki kazi za fasihi, kwa kuwa katika kazi za fasihi kuna mwingiliano baina ya kazi za fasihi na zisizo za fasihi. Pia, Wanauhistoria Mpya wanasisitiza umuhimu wa uhusiano uliopo kati ya fasihi na historia. Hivyo, katika uchambuzi huu tumeongozwa na mihimili ya nadharia ya Uhistoria Mpya ili kubaini dhima ya ushairi wa Mathias Mnyampala katika kuhifadhi historia ya jamii ya Tanzania.

## Nadharia ya Uhistoria Mpya

Nadharia ya Uhistoria mpya inaeleza uhusiano uliopo kati ya historia na fasihi. Wanahistoria Mpya wanaangalia upya mpaka uliopo baina ya historia na fasihi. Kwa kufanya hivyo wanatofautiana na wanaumbuji na wanausasaleo ambao wanasisitiza kutohusiana kwa taaluma hizi mbili. Inakubalika kwamba wahakiki wa uhistoria mpya wa Kimarekani ndio wanaotambulika kwa kueneza mkabala wa uhistoria katika fasihi katika miaka ya 1980 na ile ya 1990 (Greenblatt, 1980; Butler, 1987 na Montrose, 1999). Aidha, wanadai kuwa wahakiki wa Uhistoria Mpya walisoma matini za kifasihi kama zao la kitu kinachotokana na mazingira ya kipindi mahususi cha kihistoria. Wanauhistoria Mpya wanatambua umuhimu wa muktadha wa kihistoria katika uchambuzi wa kazi mbalimbali za fasihi. Wamitila (2003) anaeleza kuwa Wanauhistoria Mpya wanaamini kuwa haiwezekani kuitenganisha kazi ya fasihi na muktadha wake wa kijamii na kisiasa. Hii inatokana na imani yao kuwa kazi za kifasihi na zisizo za kifasihi huingiliana kwa njia za ki-mzunguko. Wahakiki hawa wanapinga tabia ya kuweka mpaka bainifu kati ya kazi ambazo ni za kifasihi na zisiso za kifasihi. Kwa ujumla kazi za kifasihi ni tokeo la mabadilishano changamano ya kijamii. Kwa hiyo, tunaweza kuelewa kazi za kifasihi kwa kuangalia hali na athari za mabadilishano ya kiutamaduni ambayo huzaa kazi hizo.

Wanauhistoria mpya wanapinga thamani za kiujumi za kazi za kifasihi ambazo hazijifungi kwenye wakati wake au muktadha wake wa kiasili; yaani hawakubaliani na ujumi mbao unavuka mipaka ya wakati. Misingi ya Nadharia ya Uhistoria Mpya inapatikana katika mawazo yao RaymondWilliams (1977), Michel Foucault, (1972, 1977, 1997) na Greenblatt, (1980). Wataalamu hawa wanasisitiza kuwa nadharia ya Uhistoria Mpya huzingatia muktadha wa kazi za fasihi katika uhakiki wa kazi husika. Mintarafu ya nadharia hii, fasihi na kazi zake haziwezi kutengwa na historia inayohusika nayokwa kuwa inairejelea, nayo inarejelewa na vitu kwenye mazingira.Aidha, nadharia hii inasisitiza umuhimu wa muktadha katika uhakiki wa kazi yoyote ya fasihi ukiwemo ushairi. Kutokana na hali hiyo, katika makala haya tunatumia baadhi ya vipengele vya muktadha wa kijamii na kisiasa uliokuwepo wakati huo kuelezea dhima za ushairi wa Mnyampala katika historia ya jamii yake.

**Muktadha wa Uandishi wa Kazi za Ushairi za Mathias Mnyampala**

Muktadha ni mazingira ya kihistoria, kijiografia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutendaji yaliyozua utungo husika. Muktadha pia hurejelea mambo yaliyomzunguka mwandishi wakati wa utungaji wake na kufichua masuala muhimu ya kazi ya fasihi katika viwango vya fani na maudhui. Aidha, kupitia kwa muktadha wa utungaji, mhakiki huelewa dhima na dhamira za mtunzi husika kupitia kwa kazi zake (Njogu na Chimera, 1999; Mumbo na Indede, 2004). Hivyo kutokana na mawazo ya wataalamu hao, kuna aina mbalimbali za miktadha katika uandishi wa kazi yoyote ya fasihi. Baadhi ya miktadha hiyo ni ya kijamii, kiutendaji, kisiasa, kijografia, kiwakati na kiuchumi. Hivyo, kazi za ushairi za Mathias Mnyampala zimesawiri miktadha mbalimbali. Mojawapo ya miktadha hiyo ni ya kihistoria, kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kwa mujibu wa Friedrich (1986), muktadha ni suala linalohusu mazingira yanayomzunguka binadamu ama mwandishi wakati wa uandishi wa kazi husika. Naye, Walibora (2007) anaeleza kuwa watunzi wa vizazi vyote waliochagua kutumia Kiswahili kama nyenzo ya kusambazia mawazo na hisia zao walikuwa wakiandika mambo yaliyokuwa yanaendana na nyakati na mazingira yao. Watunzi waliweza kutunga kazi zao kwa kufuata matukio mbalimbali ya kihistoria na kijamii yaliyokuwepo wakati huo.

Muktadha wa utunzi wa kazi za ushairi wa Mnyampala kwa kiasi kikubwa ulitawaliwa na masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ambayo kwa kweli ndiyo yanatupa muktadha wa kihistoria. Hii ni kwa sababu historia inahusu matukio au visa vinavyotokea katika maisha ya jamii maalum katika nyanja mbalimbali katika kipindi maalum cha maisha ya jamii hiyo. Katika kuzungumzia muktadha wa kazi za Mnyampala, huwezi kukwepa muktadha wa kihistoria. Hivyo basi katika kujadili muktadha wa kijamii, kisiasa na kiuchumi ndani yake kuna muktadha wa kihistoria. Kwa hiyo ili kubaini dhima za kihistoria katika kazi za ushairi za Mnyampala katika makala haya tumejadili dhima za kihistoria katika kazi za ushairi za Mnyampala kwa kujikita katika vipengele mbalimbali vya muktadha wa kijamii na kisiasa. Kwa kuwa mwandishi katika uandishi wake huangazia dhamira mbalimbali zilizomo katika muktadha unaomzunguka ili kuyawasilisha kwa hadhira na kuwasilisha kwa jamii

lengwa. King'ei na Kemoli (2001) wanadai kuwa, msanii huumba ama hutunga kazi yake kwa kuchochewa na mazingira pamoja na maudhui ya jamii anamoishi. Kutokana na mawazo ya King'ei na Kemboli, ni dhahiri kuwa uandishi wa Mnyampala ulichochewa na muktadha uliokuwepo kabla na wakati alipokuwa anaandika kazi zake. Ni bayana kuwa Mnyampala aliifahamu vizuri jamii yake ya Wagogo na nchi yake ya Tanzania kwa ujumla kutokana na masuala anayoyaangazia katika kazi zake za ushairi wa Kiswahili. Baadhi ya masuala haya yanahusu harakati za kupigania uhuru, Ujamaa na kujitegemea kwa wananchi wa Tanzania. Kwa ujumla masuala haya yana dhima kubwa ya kuhifadhi historia ya jamii ya Tanzania.

**Dhima ya Ushairi wa Mnyampala katika Kuhifadhi Historia ya Jamii**

Ushairi wa Kiswahili kama utanzu mmojawapo wa fasihi, una dhima mbalimbali katika jamii. Baadhi ya dhima hizo ni kuhifadhi historia ya jamii, kukuza ushujaa, ujasiri na kuhimiza uzalendo miongoni mwa wanajamii. Hali kadhalika, ushairi wa Kiswahili huadilisha, huburudisha, hukuza lugha na kuhifadhi amali za jamii na utamaduni wake. Katika makala haya tunajikita katika dhima moja tu ambayo ni kuhifadhi historia ya jamii. Samwel na wenzake (2013) wanaeleza kuwa katika fasihi dhima ya uhifadhi wa historia imewashughulisha wanafasihi wengi. Wanaeleza kuwa wapo wanaoona kwamba kazi ya fasihi ipo mbali sana na ukweli wa kihistoria. Wao wanaona kwamba jamii inayosawiriwa na kazi za kifasihi na jamii halisi ni vitu viwili tofauti kabisa. Kwa mujibu wa dai hili, kazi ya fasihi haibebi historia au matukio halisi ya jamii husika. Wanaounga mkono dai hili ni Lord Raglan na G. Innes kama inavyoonekana katika Raglan (1956) na Innes (1974). Samwel na wenzake (2013) wanadai kuwa Vansina (1965) na Johnson (1978) wanaeleza kwamba historia inayosawiriwa katika kazi za kifasihi si halisi bali ni yenye ukweli pendelevu inayokusudiwa kutimiza malengo ya jamii husika (Vansina, 1965 na Johnson, 1978). Hata hivyo inakubalika miongoni mwa wanahistoria kwamba ni vigumu kuwa na historia yenye ukweli thabiti kwa sababu kila mwandishi wa historia huweza kuathiriwa na itikadi au mtazamo fulani wa kijamii anaoupendelea (Samwel na wenzake, 2013). Kutokana na mawazo ya wataalamu hao tunatambua kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya fasihi na historia ya jamii. Kwa upande wa fasihi ya Kiswahili hususani ushairi wa Kiswahili, waandishi wengi huandika kazi zao kwa kusawiri historia ya jamii mbalimbali za nchi zao. Kwa mfano *Mashairi ya Azimio la Arusha* (1971) yaliyohaririwa na Grant Kamenju na Farouk Topan na ya Mnyampala (1970, 1971) yanasawiri masuala ya Azimio na siasa za Ujamaa na Kujitegemea. Aidha, hapa tumejikita kujadili dhima za ushairi wa Kiswahili katika kuhifadhi historia ya jamii kwa kuegemea katika kazi za ushairi za Mathias Mnyampala. Kwa ujumla, kazi za ushairi za Mnyampala zinasawiri ukweli wa kihistoria wa nchi ya Tanzania. Mnyampala ameandika kazi zake kwa kujikita katika muktadha uliokuwepo kabla wakati huo. Katika kujadili dhima za ushairi wa Mnyampala katika kuhifadhi historia ya jamii tumejikita katika kuangazia uhuru wa nchi ya Tanzania, Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Azimio la Arusha na kushamiri kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili. Dhima hizo zinaingiliana na kukamilishana kimuktadha ndani ya kazi husika.

## Harakati za Kupigania Uhuru na Kipindi cha Uhuru

Uhuru wa nchi ya Tanzania ni mojawapo ya dhima ya kihistoria inayojitokeza katika kazi za Ushairi za Mathias Mnyampala. Mnyampala katika kuelezea dhima hiyo ya kihistoria, ametunga mashairi mbalimbali yenye kuelezea masuala ya uhuru na matazamio ya wanajamii baada ya kupata uhuru. Pia, Mnyampala amezungumzia sifa za viongozi waliotarajiwa kuongoza nchi baada ya uhuru. Hawa ni viongozi waliotakiwa kuwatumikia wananchi katika kuleta maendeleo kwa nchi zao, bila kuwepo na ubaguzi wowote. Mfano wa mashairi yanayozungumzia harakati za kupigania uhuru na kipindi cha uhuru, katika *Diwani ya Mnyampala*, ni shairi la "Yapi Yawele 1959?" (uk. 90), "1960 Madaraka Tumebeba" (uk. 91) "Ni Madaraka Kamili" (uk. 139), "Mola Dumisha Amani" (uk. 140), "Uhuru una Kiungo" (uk. 143). Mashairi hayo yanaelezea chama cha TANU na siasa zake, yanaeleza kinagaubaga jinsi TANU ilivyoanza, kukua na kuenea kwake, wakati wa mapambano na kufanikiwa kwa TANU, uhuru na baada ya uhuru. Mashairi haya yanatoa historia ya jamii ya Tanzania. Hivyo kupitia mashairi haya, matukio ya kihistoria yanathibitika. Ni bayana kuwa kila utungo wa kifasihi (pamoja na ushairi) ni zao la jumuia fulani ambapo kiwango cha utamaduni wake, maendeleo ya fasihi yake kwa ujumla miongoni mwamambo mengine, yote huchangamana na kukamilishana ili kutupa maana maalum.

Katika kipindi cha uhuru na baada ya uhuru mashairi mengi yalitungwa yakilenga kushangilia uhuru na kuwapongeza viongozi kupigania uhuru. Mashairi ya namna hiyo yanapatikana katika kazi za ushairi za Mathias Mnyampala. Mfano mzuri ni katika *Diwani ya Mnyampala*, shairi la "Yapi Yawele 1959?" (uk. 90), ubeti wa nane usemao:

> Madaraka mng'an'ano, pato letu lifikile,
> Za madaraka yano, si fumba la kolekole,
> Tuyahozi mfatano, bure wasione gele,
> Yaliyopita si ndwele, tugange yanayokuja.

Shairi hilo linatoa historia ya Tanzania wakati wa kupigania uhuru chini ya chama cha TANU. Kadhalika katika shairi la "Mungu Muongoze Rubani" (uk. 137), "Ni Madaraka Kamili" (uk. 139), "Mola Dumisha Amani" (uk.141) na "Uhuru Uwe na Heri" (uk. 144) yametungwa kutokana na muktadha wa uhuru ambapo Mnyampala anamsifu Mwalimu Nyerere kwa kupigania uhuru kwa amani na anaiombea nchi ya Tanzania uhuru uwe wa amani. Aidha katika mashairi hayo, tunapata historia ya Tanzania ya kipindi cha uhuru.

Harakati za ujenzi wa jamii mpya ni masuala yanayozungumziwa na mtaalamu huyu katika maandishi yake. Masuala haya yalitamalaki katika kipindi cha uhuru na baada ya uhuru. Viongozi walisisitiza masuala ya ujenzi wa jamii mpya kupitia elimu ili watu waweze kujitambua na kuleta mabadiliko katika jamii. Nyerere (1967) anaeleza kuwa hatua ya kwanza ya kujenga jamii zetu ni kutoa elimu na watu kujifunza ili waweze kutambua kuwa wao ni akina nani na wana jukumu gani katika kuleta maendeleo ya jamii zao. Hivyo, katika kipindi hicho, elimu ilisisitizwa sana ili kuweza kujenga jamii mpya inayojitegemea katika nyanja zote. Kwa hivyo dhamira ya ujenzi wa jamii mpya ambayo inadhihirika katika tungo za kishairi zinaakisi yaliyohimizwa

katika taifa la Tanzania wakati huo na hivyo tungo hizi zinakuwa ghala la kuhifadhi historia ya jamii.

Mashairi hayo yanaonesha kuwa yalitungwa katika kipindi cha uhuru na katika kipindi hicho waandishi walitunga mashairi yanayolenga kuhamasisha amani, umoja na uongozi bora. Katika mashairi hayo, Mnyampala anamsifu Rais wa kwanza wa Tanzania Mwalimu Nyerere kwa kupigania uhuru kwa amani. Mashairi hayo yana dhima kubwa ya kuhifadhi historia ya taifa la Tanzania wakati wa kupigania uhuru na uhuru wenyewe. Kadhalika, katika mswada wa *Mashairi ya Vidato*, shairi la "Kauwawa Kennedy", ubeti wa sita usemao.

> Yuko wapi Mahatma, wa India Mashariki,
> Ijapo alisimama, hadi kujitia dhiki,
> Hakuambua la wema, kauawa hamaki,
> Tunakuomba Maliki, umrehemu Kennedy. (uk. 5)

Katika shairi hili Mnyampala anamzungumzia Kennedy ambaye alikuwa Rais wa nchi ya Marekani aliyeuawa mwaka 1963 huko Marekani. Kennedy alikuwa kiongozi mwenye umri mdogo aliyekuwa na hekima na mwenye kufuata misingi ya utu wa binadamu na asiyependa ubaguzi wa rangi tofauti na misingi ya wakoloni waliyokuwa nayo. Kupitia kwa shairi hili, mwandishi anapinga ubaguzi wa rangi, ukandamizaji, unyonyaji na uoneaji. Mwandishi anasisitiza suala la uzalendo wa viongozi, uwajibikaji wa viongozi, wenye kupinga ubaguzi, wapenda amani ndani ya nchi zao, viongozi ambao hawatumii utawala wa mabavu ambao unaleta machafuko katika nchi. Kupitia kwa shairi hili tunapata historia ya maisha ya Rais Kennedy na nchi ya Marekani miaka ya 1960. Kwa ujumla maandishi yenye hisia hizo na historia za watu mashujaa waliopinga udhalimu huo yanatuwezesha kujua historia za nchi za Magharibi na kipindi cha uhuru wa nchi za dunia ya tatu (Kiafrika). Kwa hiyo, waandishi waliweza kutumia mifano mbalimbali ya watu maarufu wenye uzalendo katika nchi zao na kuwa kielelezo katika nchi zinazoendelea zilizokuwa zinapata uhuru miaka ya 1960. Kutokana na nukuu hiyo, ni wazi kuwa kwa muda mfupi tunaweza kujifunza mambo mengi ya kihistoria kupitia ushairi wa Mnyampala. Vilevile katika shairi hilo mwandishi alihusisha tabia za Kennedy na tabia za Nyerere ambaye alikuwa Rais anayejali usawa wa watu wote katika jamii mara baada ya uhuru wa Tanzania.

Mnyampala ameeleza masuala ya uhuru katika shairi la "Kitung'ati" (uk. 7), katika shairi hilo anaeleza namna ambavyo viongozi walipambana kupigania uhuru wa nchi ya Tanzania hadi kufanikiwa. Hapa Mnyampala anazungumzia suala zima la uhuru na viongozi wazalendo wa nchi nyingi zilizopata uhuru miaka ya 1950 na 1960. Kwa mfano, Rais Nyerere, Lumumba wa Kongo na Nkrumah wa Ghana wakati huo walijitokeza na kutetea haki za Mwafrika. Kupitia shairi hili tunapata historia ya nchi za Afrika wakati wa kupinga udhalimu wa kikoloni na kupigania uhuru wa nchi za Afrika. Hivyo Mnyampala katika shairi hilo anazungumzia uzalendo wa viongozi wakati huo katika kupambana kuleta uhuru katika nchi zao.

Kadhalika, Mnyampala katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* na *2*, ameelezea kinagaubaga historia ya nchi ya Tanzania. Kwa mfano, katika *Ngonjera za UKUTA Na.*

*1*, kuna ngonjera za kusifu harakati za kupigania uhuru na kukumbuka sikukuu za Taifa. Katika kitabu hicho, Mnyampala ameeleza sikukuu ya kuzaliwa kwa chama cha TANU, 7 Julai 1954, katika ngonjera ya "Ni Saba Saba ya ngapi?" (uk. 68-70). Kwa ujumla, kipindi hicho kilikuwa ni wakati ambao mambo mbalimbali yalifanyika nchini Tanganyika mara baada ya uhuru. Pia, amezungumzia sikukuu ya Jamhuri ya Taifa, 9 Desemba 1961 katika ngonjera ya "Sikukuu za Jamhuri" (uk. 65-66), katika ngonjera ya "Sikukuu ya Mwungano" (uk. 66-67) pia ngonjera hiyo imezungumzia siku ya muungano, 26 Aprili 1964. Suala la muungano limejitokeza pia katika kitabu cha *Diwani ya Mnyampala* Kwa ujumla ngonjera hizo zinatusaidia kuelewa historia ya vyama vyetu. Ngonjera hizo zinazungumzia kinaganaga historia ya nchi ya Tanzania kwa kutumia sikukuu za Taifa.

Vilevile, *Ngonjera za UKUTA Na. 1* kuna ngonjera zinazohusu Viongozi Wetu (uk. 25-35). Katika ngonjera hizo Mnyampala anaelezea wasifu wa viongozi wa kisiasa wa awamu ya kwanza nchini Tanzania, kuanzia Baba wa Taifa hadi mawaziri wake wote. Ngonjera hizo zinatusaidia kuelewa sifa za viongozi na chama cha TANU. Pia ngonjera hizo zinaonyesha imani na upendo wa wananchi kwa viongozi wao. Aidha, ngonjera hizi ni hifadhi kubwa ya historia ya nchi ya Tanzania kuanzia harakati za kupigania uhuru, wakati wa uhuru, baada ya uhuru pamoja na wasifu wa viongozi wa kwanza wa Tanzania na siasa za nchi yake. Kwa kuwa kipindi hicho kauli nyingi za kisiasa alizozitoa Mwl Nyerere, Mnyampala aliweza kuzitungia mashairi, na kusaidia kutangaza siasa za nchi yake kwa wanajamii. Kupitia kazi za ushairi za Mnyampala zinatuingiza kinaganaga katika mjadala wa kipindi cha kupigania uhuru, uhuru na baada ya uhuru. Kwa kufanya hivyo kazi za ushairi za Mnyampala zimekuwa na dhima kubwa ya kuhifadhi historia ya nchi ya Tanzania na jamii kwa ujumla.

**Muungano wa Tanganyika na Zanzibar**

Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulifanyika tarehe 26/04/1964. Tukio hili lilifanyika baada ya Tanganyika na Zanzibar kupata uhuru kutoka kwa wakoloni ambao walitawala miaka mingi katika nchi hizo. Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni mojawapo ya matukio ya kihistoria yaliyofanyika mwaka 1964. Hivyo, kutokana na hali hiyo, waandishi wengi wa kipindi hicho waliandika kazi zao wakigusia masuala ya muungano kwa kuwa ndilo jambo lililokuwa linavuma wakati huo. Mnyampala kama mmoja wa waandishi mashuhuri naye aliathiriwa na masuala ya muungano. Hakuwa nyuma katika kutunga mashairi yaliyokuwa yanaelezea masuala ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Aidha, katika *Diwani ya Mnyampala* shairi la "Muungano Utupambe" (uk. 147), Mnyampala anaomba Mungu muungano uwe wa amani na kushirikiana kwa pamoja bila kuwepo na mikwaruzo wala vita baina ya nchi hizo. Kwa hiyo ni dhahiri kuwa kuna uhusiano kati ya fasihi na historia ya jamii katika mashairi ya Mnyampala. Hivyo kupitia mashairi ya Mnyampala historia ya Tanzania inajidhihilisha.

Katika mswada wa *Mashairi ya Vidato* shairi la "Tanzania ya Amani" (uk. 9), linazungumzia masuala ya muungano. Shairi hili liliandikwa tarehe 10/07/1966 baada

ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambao ulikuwa tarehe 26/04/1964. Ubeti wa sita wa shairi hilo unasema:

Tuliungana pamoja, wa visiwani na bara,
Tanganyika na Unguja, Mwungano wetu imara,
Lakini wao wangoja, hadi waende ahera,
Hebu itie fikira, na yetu vinafanana? (uk. 9)

Mwandishi katika ubeti huo anasawiri masuala ya muungano wa bara na visiwa na anaeleza kuwa muungano uliopo ni imara na unapaswa kuheshimiwa. Mnyampala anaeleza kuwa wengine wanatamani kuungana lakini wanashindwa kwa sababu ya kukosa mwelekeo. Pia, masuala ya muungano yamezungumziwa katika shairi la "Kitung'ati" (uk. 7) ubeti wa tano ambapo mtunzi anaeleza kuwa:

Nguvu-moja ya kukata, ya Tanzania mirija,
Tukate bila kusita, tangu bara na Unguja,
Kazi-yetu ni kupata, pato letu la pamoja!
Kawa alivyoitaja, mtukufu wa KITUNG'ATI.

Katika ubeti huu historia ya muungano inabainika kwa kuelezea malengo ya muungano. Mnyampala anaeleza kuwa malengo ya muungano huo ni kuwapo kwa pato la pamoja, kuondoa ubaguzi na kuwa na nguvu moja katika kuimarisha uchumi wa muungano wa Jamhuri ya Tanzania. Kutokana na mashairi hayo ni dhahiri kuwa waandishi hutunga kazi zao kwa kuzingatia muktadha husika. Watunzi wa fasihi huchota maudhui yaliyomo katika jamii na kuyaweka katika sanaa kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusiana na mambo yanayoendelea katika jamii. Mambo hayo huwasilishwa kisanaa kiasi kwamba hadhira inaelimishwa na wakati huohuo inapata burudani.

Muktadha huu wa muungano pia umesawiriwa katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1*, mfano ngonjera ya "Sikukuu ya Muungano" (uk. 66-67). Kama asemavyo mwandishi katika ngonjera hiyo:

*Sikukuu ya muungano ni siku ya kusherekea kuungana kwa Tanganyika na Zanzibar baada ya kutawaliwa na wakoloni miaka mingi. Tarehe yake ilikuwa ni 26 Aprili, 1964. Ngonjera ifuatayo inazungumzia sikukuu hiyo*:

Mwananchi
Nasikia sikukuu, hii ndiyo sikukuu gani?
Wahutubia wakuu, pembe zote humu nchini
Nena nami ninukuu, na niyaweke kichwani
Mwungano ni siku gani, wanayosema wakubwa? (Ubeti wa kwanza)

Mwanasiasa
Siku tunajivunia, sisi sote humu nchini
Sote tukaungania, Unguja hadi Barani
Unguja iliingia, na Tanganyika ushoni
Sikukuu yenye shani, ya kuunda Tanzania (ubeti wa nne)

Dondoo hili linaonesha uhalisi wa historia ya Tanzania. Hapa mwandishi ametumia ngonjera hiyo kutupa picha kamili ya historia ya Tanzania. Hii ni kutokana na ukweli kwamba maelezo haya yanaweza kuthibitishwa kutoka katika vyanzo vingine. Huu pia, ni ukweli kwamba waandishi wa ushairi huwa hawaandiki kutoka hewani au angani, kwani kwa kiasi kikubwa huathiriwa na mazingira au historia ya jamii husika. Katika ngonjera hii mtunzi anatuingiza katika kujua masuala ya uhuru na mambo yaliyotokea baada ya uhuru. Mnyampala anazungumzia Muungano baina ya Unguja na Tanganyika na kuunda Tanzania. Hivyo kupitia ngonjera hiyo tunapata historia ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar uliotokea mwaka 1964 na kusudi la muungano huo.

**Azimio la Arusha**

Katika kazi za ushairi za Mnyampala, ameongelea pia masuala ya Azimio la Arusha mwaka 1967. Azimio hilo liliambatana na siasa ya ujamaa na kujitegemea lililotangazwa mwaka huo na kuleta sura mpya ya ushairi wa Kiswahili. Mfano mzuri wa mashairi haya unapatikana katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* na *2*. Ngonjera hizo zinazungumzia masuala ya azimio la Arusha na sera zake. Ujamaa na Kujitegemea ni masuala yaliyoshamiri miaka ya 1960 mara baada ya uhuru wa Tanzania. Ujamaa na Kujitegemea ni sera iliyokuwa ikienezwa chini ya mwamvuli wa Azimio la Arusha. Masuala ya Ujamaa na Kujitegemea yanajitokeza vyema katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* na *2* na umesawiriwa kwa kiasi kidogo katika mswada wa *Mashairi ya Vidato*. *Mashairi ya Vidato* ni mswada ulioandikwa kipindi cha vuguvugu la siasa ya Ujamaa ambayo ilikuwa ikienezwa chini ya mwamvuli wa Azimio la Arusha. Azimio hili lilianzishwa mwaka 1967 chini ya uongozi wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Azimio la Arusha lilikusudia kuleta haki sawa kwa wote pamoja na kuinua uchumi wa nchi na wanajamii kwa ujumla.

Mswada wa *Mashairi ya Vidato*, Mnyampala anasisitiza kuheshimu na kulinda siasa za ujamaa. Kwa hiyo baadhi ya mashairi yaliyomo katika mswada wa *Mashairi ya Vidato* yanahusu masuala ya Ujamaa na Kujitegemea. Mfano wa mashairi yaliyogusia masuala ya Ujamaa ni shairi la "Saba-Saba" (uk. 3), "Tanzania ya Amani" (uk. 9), na "Uaminifu" (uk. 1). Aidha kupitia kwa mashairi haya, tunapata picha kamili ya mapitio ya historia ya nchi ya Tanzania tangu 1954-1967. Mfano shairi la "Uaminifu" linaeleza kuhusu siasa ya Ujamaa na Kujitegemea kama vile kuepuka misaada inayovunja siasa za nchi zinazoendelea ama zilizotoka kupata uhuru. Aidha, katika shairi la "Kitung'ati[1]" (uk. 7) Mnyampala anaeleza jinsi baba wa Taifa Mwalimu Nyerere alivyokuwa anatangaza siasa za ujamaa. Masuala haya yanajitokeza waziwazi kupitia ubeti wa sita. Mwandishi anasema:

---

[1] Kitung'ati ni mtu shujaa sana mwenye elimu ya kuongoza majeshi yake, mwenye shabaha na hatimaye kufaulu katika vita. Mtu huyo akipangiwa jambo wafuasi wake wanaamini kuwa bila shaka watafaulu tu, na kwa kweli wanafaulu (Mnyampala, 1967).

Nguvu-moja ndiyo haja, siasa ya Ujamaa,
Sawa sawa wote waja, tabaka moja kukaa,
Kazi-yetu ni kuchuja, na kupunguza tamaa,
Kama alivyoandaa, Mwalimu wa KITUNG'ATI. (uk. 7)

Hapo mwandishi anazungumzia sera za siasa ya ujamaa inayosisitiza usawa wa binadamu, kuondoa matabaka katika jamii, kuchukua mambo mazuri yanayoleta maendeleo katika nchi na kupunguza tamaa ya vitu mbalimbali vinavyodidimiza uchumi wa nchi. Kadhalika, Mnyampala katika ubeti wa saba anazungumzia masuala ya kujitegemea na anasisitiza watu kufanya kazi kwa nguvu na kuleta maendeleo ya nchi na jamii kwa ujumla. Kadhalika katika sera ya Ujamaa, Mwalimu Nyerere alikuwa msitari wa mbele katika kupigana na adui watatu ambao ni ujinga, maradhi na umasikini. Hili linabainishwa katika ubeti wa kumi usemao:

Nguvu-moja kusimama, adui zetu kushinda,
Adui watatu kama, wanenepe waliokonda,
Kazi-yetu kuwachoma, tupige na kuwaponda,
Kama anavyopenda, Mtukufu KITUNG'ATI. (uk. 7)

Katika ubeti huu Mnyampala anaeleza kwamba Rais Nyerere alikuwa anawataka wananchi kushirikiana katika kupambana na maadui watatu. Kupitia mashairi haya tunapata kujua historia halisi ya siasa za Tanzania miaka ya 1960, ambazo zilikuwa ni kupambana kwa pamoja katika kuondoa umasikini, maradhi na ubaguzi.

Hali kadhalika, *Ngonjera za UKUTA Na. 1* na *2* zinasawiri vyema siasa ya Ujamaa na Kujitegemea pamoja na Azimio la Arusha matukio ambayo ni ya kihistoria nchini Tanzania. Kwa mfano katika *Ngonjera za UKUTA Na. 1* kuna ngonjera za "Utukufu wa Taifa" (uk. 12-18) zinazofafanua maadui watatu ambao ni ujinga, umasikini na maradhi. Kwa ujumla, *Ngonjera za UKUTA Na. 1* na *2*, zilitungwa kipindi cha Azimio la Arusha na kuchapwa mwaka 1970 na 1971. Mwandishi ametunga mashairi yake kwa kuegemea katika masuala ya kisiasa yaliyokuwepo wakati huo, hususani siasa za TANU (chama kilichoanzishwa mwaka 1954) na Azimio la Arusha lililoanzishwa mwaka 1967. Kadhalika utunzi wa ngonjera ni mojawapo ya matukio ya kihistoria. Kwa kuwa masuala ya Ujamaa na Kujitegemea yalichangia kufufua mtindo huu wa mashairi ya ngonjera kwa lengo la kuwezesha wanafunzi na jamii kwa ujumla kufahamu siasa iliyokuwepo katika nchi yao kwa namna ya uigizaji wa vitendo halisi. Kipindi hicho Nyerere ndiye alitoa rai kwa waandishi kutunga kazi za fasihi zinazotangaza sera ya Azimio la Arusha ili jamii iweze kuelewa sera hiyo vizuri. Kama aelezavyo Mnyampala (1971:3) katika dibaji yake kuwa fani ya ngonjera ilipatiwa msukumo kwa mara ya kwanza na Mwalimu Nyerere, kama aelezavyo hapa:

> Ngonjera hizi nimezitunga kwa ajili ya Azimio la Arusha ili lipate kutangazwa zaidi kwa njia hii na, hasa kwa ajili ya kutekeleza maagizo ya Mtukufu Mwalimu Julius K. Nyerere aliyotuagiza wakati alipotuita washairi wote wa Kiswahili, tukaonane naye Ikulu tarehe 6 Juni, 1968. Siku hiyo Mwalimu alisema, "Tangazeni Azimio la Arusha, na kutukuza Utamaduni wa Taifa letu".

Kutokana na maneno hayo ni dhahiri kwamba ngonjera hizi ziliandikwa kwa lengo la kuelimisha wanajamii kuhusu siasa za Ujamaa na Kujitegemea na kutukuza utamaduni wa taifa la Tanzania kwa dhati. Kutokana na maelezo ya Mnyampala, tunaweza kusema kuwa lisingelikuwepo Azimio la Arusha, labda hata fani ya ngonjera ingelikuwa bado imefifia. Aidha, ngonjera zilipata umbo jipya kutokana na mabadiliko ya kijamii na kisiasa yaliyokuwepo wakati huo. Kama asemavyo Greenblatt (1980), kila mtunzihuwa ameathiriwa na mazingira yake na athari hizi hazina budi kujitokeza katika utunziwake.Hivyo, kupitia mashairi ya ngonjera za Mnyampala zinatuwezesha kupata historia ya nchi ya Tanzania.

**Kushamiri kwa Matumizi ya Kiswahili**

Lugha ya Kiswahili ilianza kushamiri zaidi wakati wa kupigania uhuru nchini Tanzania miaka ya 1960. Kiswahili kilitumika kuwaunganisha Watanzania katika kupigania uhuru wa nchi yao. Miaka ya 1960, waandishi mbalimbali walihamasishwa kutumia Kiswahili katika utunzi wa kazi zao za fasihi. Mnyampala ni mmojawapo wa waandishi waliokuwa msitari wa mbele kutumia lugha ya Kiswahili katika utunzi wa kazi zake. Kama asemavyo Abdulaziz (1969), Mnyampala alikuwa anakereka sana na matumizi ya lugha ya kigeni mahala ambapo hapana sababu ya kuitumia. Hivyo alipendekeza Halimashauri Kuu ya UKUTA itayarishe 'Operation Kiswahili'. Abdulaziz anaeleza kuwa "kwa bahati mbaya 'Operation Kiswahili' haikufanyika katika uhai wa Mnyampala" (uk. 2). Mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti na jamaa wa karibu wa Mnyampala[2] yanadhihirisha kuwa Mnyampala akiwa diwani miaka ya 1960 aliishawishi serikali na kusababisha majina ya barabara na mitaa yaliyokuwa yameandikwa kwa lugha ya Kiingereza mjini Dodoma yaondolewe na kuandikwa kwa Kiswahili. Wito huo uliitikiwa na Halmashauri ya Mji wa Dodoma ilichukua hatua ya kufuta majina mengi ya barabara na mitaa yaliyokuwa yameandikwa kwa Kiingereza na yakaandikwa kwa Kiswahili[3].

Mifano ya majina ya mitaa na barabara yaliyokuwa yameandikwa kwa Kiswahili kutokana na ushauri wa Mnyampala ni kama: Mtaa wa Hatibu, Mtaa wa Madeneni, Mtaa wa Jamatini, Mtaa wa Nyerere, Barabara ya Sabasaba, Barabara ya Kikuyu, Barabara ya Hospitali na Barabara ya Keeka (Makaka, 2012)[4]. Kadhalika, Mnyampala alikuwa mzalendo wa kutumia lugha ya Kiswahili katika utunzi wa kazi zake za ushairi, nathari, hadithi na nyinginezo. Kama aelezavyo Abdulaziz (1969), Mnyampala

[2] Mahojiano hayo yalifanywa baina ya mtafiti na Balozi Jobu Lusinde, nyumbani kwake Kilimani, Dodoma. Tarehe 12/05/2017.

[3] Taarifa hizi tulizipata katika mahojiano yaliyofanyika baina ya mtafiti na jamaa wa karibu waliofanya kazi na Mathias Mnyampala kipindi cha uhai wake huko Dodoma. Tarehe 12/05/2017.

[4] Maelezo haya yaliyotolewa na Makaka tuliweza kuyathibitisha katika mahojiano yaliyofanyika baina ya mtafiti na watafitiwa mkoani Dodoma.

kwa upande wa lugha alikuwa anaamini kwa dhati kuwa lugha ya taifa, yaani Kiswahili, huhimili mazingira yote ya kitaifa. Hii ndiyo maana Mnyampala ameandika kazi zake kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Hivyo basi, kipindi ambacho kazi za Mnyampala zinaandikwa kulikuwa na kampeni ya kueneza na kukuza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Wakati huu ulikuwa ni kipindi cha kupigania uhuru miaka ya 1960, ambapo lugha ya Kiswahili ndiyo ilikuwa ikiwaunganisha wananchi wakati wa kudai uhuru wa nchi hiyo. Kadhalika, kilikuwa kipindi cha kushamiri kwa fasihi andishi na kudumaa kwa fasihi simulizi. Rais Julius K. Nyerere pamoja na makamu wake wa pili Rashidi Mfaume Kawawa mwaka 1967 walitangaza Kiswahili kuwa lugha ya taifa ya Tanzania. Kutokana na tamko hilo, kazi mbalimbali za kigeni zilitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na waandishi wa fasihi akiwemo Mnyampala walihamasishwa kuandika kazi zao kwa lugha ya Kiswahili. Mathalani, Mnyampala katika *Diwani ya Mnyampala*, anahamasisha wanajamii kuenzi Kiswahili kwa kutunga shairi liitwalo, "Lugha Yetu Kiswahili" (uk. 123). Shairi hilo linaeleza umuhimu wa kuenzi na kutumia lugha za kienyeji na Kiswahili. Pia katika kitabu chake cha *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Washairi*, kuna shairi lake linalohusu Kiswahili linaloitwa "Johari ya Tanganyika". Katika shairi hilo, Mnyampala anasifu washairi na lugha ya Kiswahili. Huu ni wakati ambapo taasisi mbalimbali zilizojihusisha katika kukuza lugha ya Kiswahili zilianzishwa, kwa mfano taasisi ya Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili mwaka 1962 na baadaye TUKI mwaka 1970, UKUTA mwaka 1967 na BAKITA mwaka1967. Isitoshe, Mnyampala amezungumzia Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili na umuhimu wake katika kukuza lugha ya Kiswahili katika *Mashairi ya Vidato*, shairi la "Jarida la Kiswahili" (uk. 9). Hivyo, kupitia mashairi hayo tunapata kuelewa jitihada zilizofanyika katika kukuza na kueneza Kiswahili pamoja na historia ya asasi na taasisi za Kiswahili.

Majarida na magazeti mbalimbali yalianzishwa miaka ya 1950 na 1960 kwa lengo la kukuza na kuendeleza Kiswahili na kuwawezesha waandishi wa ushairi na fasihi kwa ujumla kuandika kazi zao na kuziweka humo ili ziweze kusomwa na wananchi. Mfano wa magazeti hayo ni *Mambo Leo*, *Baragumu*, *Ngurumo* na mengine ya makabila kama vile *Bugiya*, *Gandi* na *Wela* ambamo mashairi mengi ya kisiasa yaliandikwa humo. Mnyampala ni miongoni mwa waandishi walioandika kazi zao katika magazeti mbalimbali yaliyokuwepo wakati huo. Hili linajidhihilisha zaidi katika kitabu chake cha *Diwani ya Mnyampala* (uk. 66-69), Mnyampala ameandika mashairi yanayohusu gazeti la *Mwananchi*. Mnyampala alitunga mashairi yake kuombea gazeti hilo na kulitakia kila la kheri. Mfano wa mashairi hayo ni "*Mwananchi* Usonge Mbele" (uk. 66), "*Mwananchi* Utabalaji" (uk. 67), "*Mwananchi* Kua Salama" (uk. 68) na "Johari Ninakupamba" (uk. 68). Kwa ujumla, kupitia lugha ya Kiswahili, pamoja na lugha nyingine, ushairi hutungwa, misamiati na methali huibuliwa kulingana na muktadha wa kihistoria na kijamii. Aidha, lugha huweza kutumiwa kutolea hotuba, maghani katika shughuli mbalimbali za kijamii na kuleta maendeleo ya nchi pamoja na kutunza historia ya jamii husika.

## Hitimisho

Kutokana na mjadala huu, ni dhahiri kuwa mashairi ya Mnyampala yanatupa picha kamili ya mapitio ya historia ya jamii ya nchi ya Tanzania tangu 1954 hadi miaka ya 1970. Hapa Mnyampala amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutuingiza katika kujua historia ya Tanzania kipindi hicho. Kupitia ushairi wake tunapata kumbukumbu ya historia ya nchi ya Tanzania kabla na baada ya uhuru. Kuanzia TANU, wakati wa kupigania uhuru, wakati wa uhuru na baada ya uhuru, Muungano wa Unguja (Afroshiraz) na Tanganyika (TANU) pamoja na masuala ya Azimio la Arusha lenye lengo la kuondoa unyonyaji na ukandamizaji na kuleta usawa na umoja aliowekwa chini ya Azimio la Arusha. Hivyo, kupitia ushairi wa mtaalamu huyu tunaweza kupata picha kamili ya mkoloni kama mtu mbaya, dhalimu, mnyonyaji, mkandamizaji na mwenye maonevu. Vilevile tunapata historia za watu mashujaa waliopinga unyonyaji na ukandamizaji inapatikana katika kazi za ushairi za Mnyampala. Ni dhahiri kuwa kupitia ushairi wa Mnyampala tunajifunza kuwa ushairi kama zao la jamii hubadilika kutegemeana na wakati, mazingira na muktadha. Hivyo ushairi hufuata mkondo wa kihistoria kwa kutumia vigezo vya kisiasa na kijamii. Kadhalika kupitia ushairi wa Mnyampala tunabainimabadiliko ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Pia ushairi hutusaidia kuitambua jamii husika kwa mujibu wa jitihada na changamoto zao katika kujijenga kama jamii maalum inayoweza kutambuliwa kote ulimwenguni kutokana na utamaduni wao. Utamaduni huu ni sehemu ya turathi na historia yao ambayo inaweza kupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa kweli ushairi wa Mnyampala unaweza kuangaliwa kama dafina ya historia yake na jamii ya Tanzania kwa ujumla.

**Marejeleo**

Abdulaziz, M. H. (1969). "Maisha ya Mathias Mnyampala" *Swahili.* Vol. 39/1- 2. Dar es Salaam: TUKI.

Friedrich, P. (1986). *The Princes of Naranja: An Essay in Anthrohistorical Method*. Austin: University of Texas Press.

Innes, G. (1974). *An Introduction to the African Prose Narrative*. South Africa: African World Press.

Kezilahabi, E. (1974). *Kichomi.* Nairobi: Heinemann Educational Books.

King'ei, K., na Kemoli, A. (2001). *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.

Makaka, E. E. (2012). "Mathias Mnyampala: A Multifaceted Personality". Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Jamii katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Mmbaga, N. O. (1978). "Dhima ya Ushairi katika Kuhifadhi Historia ya Jamii". Katika *Mulika Na. 14*. Dar es Salaam: TUKI.

Mnyampala, M. (1965). *Diwani ya Mnyampala*. Dar es Salaam: Oxford University Press.

_______(1968). *Mashairi ya Hekima na Malumbano ya Ushairi*. Dar es Salaam: UKUTA.

_______(1970). *Ngonjera za UKUTA Na. 1*. Dar es Salaam. Oxford University Press.

_______(1971). *Ngonjera za UKUTA Na. 2*. Dar es Salaam. Oxford University Press.

Montrose, L. (1999). *A Glossary of Literary Terms*. http://mthoyibi.files.wordpress.com/.../a-glossary-of-literary-terms-7th ed

Mumbo, C. K., na Indede, F. N. (2004). *Johari ya Kiswahili: Kidato cha Tatu*. Nairobi: Acme Press Ltd.

Mwaruka, R. (1968). *Utenzi wa Jamhuri ya Tanzania*. Nairobi: East African Bureau.

Mwinyihatibu, M. A. (1967). *Utenzi wa Uhuru wa Tanganyika*. Katika *Swahili Na. 37/1-2*. Dar es Salaam: TUKI.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadhari na Mbinu*. Nairobi: JomoKenyatta Foundation.

Nyerere, J. K. (1967). *The President Explains the Arusha Declaration*. Dar es Salaam: National Printing Co.

Raglan, L. (1956). *The Hero: A Study in Tradition, Myth and Drama*. New York. American Library.

Samwel, M., na wenzake (2013). *Ushairi wa Kiswahili: Nadharia, Maendeleo, Mwongozo kwa Walimu wa Kiswahili na Diwani ya Mea*. Dar es Salaam: MEVELI Publishers.

Topan, F., na Grant, K. (1971). *Mashairi ya Azimio la Arusha*. Dar es Salaam: Longman.

Vansina, J. (1965). *Oral Tradition: A Study in Historical Methodology*. London: Routledge & Kegan Paul.

Walibora, K. (2007). *Diwani ya Karne Mpya*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.